



Zahanati ya Charambe , iliyoko Kata ya Charambe



TEMEKE YETU

Na.014 JARIDA JULAI-DISEMBA 2017



Jengo la Ofisi ya Uendelezaji wa Miundombinu Jiji la Dar-es-Salaam -Manispaa
ya Temeke

(Dar-es-Salaam Metropolitan Development Project—DMDP)
ilizinduliwa na Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Selemani Jafo

Uongozi - Bodi ya Uhariri




Mkuu wa Wilaya Mhe. Felix Lyaniva ,
Mwenyekiti Kamati ya Ulinzi na Usalama
Wilaya ya Temeke,

Mstahiki Meya , Mhe. Abdallah J.
Chaurembo ,
Halmashauri ya Manispaa ya
Temeke
2015-2020



Mkurugenzi wa Halmashauri ya
Manispaa ya Temeke
Bw. Nassib Mmbaga



Inatoka UK 14

Lakini; aliongeza kuwa yapo maeneo machache yaliyosalia, na maeneo haya ni yale ya ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua kama vile mfereji wa kwa Shego, malipo ya fidia kwa ajili hiyo yanaandalishi na yatafanika kabla ya kumalizika mwaka huu.



Hafla ya kupokea fedha za Mkopo kutoka benki ya CRDB, kiasi ambacho kitatumika kulipia fidia maeneo yatakayopisha Mradi wa DMDP,Huo ni uthibitisho.

Akizindua mradi wa kwanza Jijini wa DMDP ambao ni ofisi na maabara; Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Selman Jaffo alisema, ninamnukuu 'rafiki zangu wa Temeke, hongereni sana kwa nyie kuwa wa kwanza



Ugawaji wa fidia kwa walengwa wa Mtaa wa Mwanamtoti , kupisha ujenzi wa barabara.

'wafanyakazi wako wanafanya kazi kwa kufuata maagizo, nami nilipoamua kuja huku sikusita kwa kuwa nilijua nakuja kwa watu makini na wanaojituma kufanya kazi hongereni sana', mwisho wa kunukuu.

Mradi wa DMDP ni mkataba wa miaka mitano 2015



Mstahiki Meya , Mhe. Abdallah Jaffari
Chaurembo

TEMEKE YAMWAGIWA SIFA

Na Edda Mmari

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Shinyanga Mh;Gulam Afidhi aimwigia sifa Manispaa ya Temeke kwa kuwa na uwazi wa mikataba na shughuli za kimaendeleo zinavyowekwa wazi kwa jamii ili kila mwananchi aweze kujua kinachoendelea katika Wilaya yao. Aliyasema hayo alipokuja kuhudhuria kikao cha ALAT Dar es Salaam, ambapo yeye ni Mwenyekiti wa kikao hicho cha ALAT ndani ya ukumbi wa Iddi Nyundo wa Manispaa ya Temeke.



Hata hivyo alikiri kujifunza kutoka kwa viongozi mahili wa Manispaa hii kwa juhudii wanazofanya kuweke uwazi wa mambo na usimamizi mzuri wa miradi hiyo.

Pongezi nyingi kwa Mstahiki Meya Abdallah Chaurembo na Mkurugenzi Mkuu wa Manispaa ya Temeke Ndgi;Nassibu Mmbaga.

Inatoka uk.13

zitakazopokelewa na Mradi wa DMDP,kati ya fedha hizo, biliioni 223 zitatumika kwa miradi 13 Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Bwana Edward Simon ni mratibu wa Mradi wa DMDP halmashauri ya manispaa ya Temeke, akizungumza mbele ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Bwana Edward alisema Miradi iliyokubalika ni Ujenzi wa Ofisi ya Utawala ya Mradi, Maabara ya kupima udongo vyote viro hapa makao makuu barabara ya Mandela na Taifa ambavyo utavizindua leo, Daraja lenye urefu wa mita 16 na barabara inayounganisha Kijichi - Toangoma yenye urefu wa kilometra 3.

Kuisha kwa barabara hii kutapunguza msongamano na kupisha wale wanaotoka nje ya mji bila kuingia katikati ya mji.

Vile vile ujenzi wa daraja na barabara ya Mwanamtoti yenye urefu wa kilometra 1.8, ambayo itaunganisha Kigamboni kuititia barabara na daraja la Kijichi -



Toangoma –hadi barabara kubwa ya Kilwa.

Temeke uionayo hivi sasa kwa miaka minne ijayo itakuwa tofauti aliongeza kusema Bwana Edward, na kuendelea; "kwani itakuwa yenye miundombini ya kimataifa, itakuwa na barabara za lami zenyte mtandao ya kilometra 160 jumla, ikiwemo barabara ya Temeke - Mbagala, Nzasa - Kilungule, barabara kumi za Mitaa na Taa za barabarani Kata ya Kijichi, kituo cha Afya Makangarawe na Kiwanja cha mchezo wa Mpira, Nyumba za makazi za bei naafuu Vikunai, mifereji ya maji ya mvua, kama vile mfereji wa Kwa shego na mfereji wa Chang'ombe.

Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke una haki ya kupon gezwa, pongozi kwa mengi, kwanza ni wasikivu, kwa masuala ya maagizo yote yanayotolewa na Serikali, kama vile katika hili, Temeke ili kuwa ya kwanza kuandaa mpango wa jinsi gani watapata fedha za kulipa fidia ili mafungu ya fedha za mradi wa

Dar-es-salaam Metropolitan Development Project-DMDP unaofadhiliwa na mfuko wa Benki ya Dunia zitolewe na mradi kuanza mara moja. Mradi huu wa kwanza ulisainiwa mwezi Februari mwaka huu 2017.



Utajji saini Mkataba wa ujenzi wa daraja na barabara ya Kijichi—Toangoma na Mkandarasi uliofanyika kati-ka eneo la Mradi

Ujenzi wa Barabara na daraja la Mwanamtoti, Barabara inayounganisha barabara ya Kilwa na Kijichi—Toangoma

Mstahiki Meya Mhe. Abdallah Chaurembo na Mkurugenzi Bwana Photidas Kagimbo mwaka 2015, walichukua jukumu la kufuta fidia kutoka benki ya CRDB na kufanikisha kupata biliioni 19.6 na milioni 700 za ziada zilitokana na mapato yetu yenye ili kukamilisha biliioni 20.3.

Bwana Edward akiwasilisha taarifa mbele ya menejimenti hivi karibuni alisema; Mradi umefanikiwa kutumia kiasi cha shilingi zaidi ya bilioni 18 kuwalipa mpaka hivi sasa,kulipa fidia wakazi 2,130 wenye nyumba ama mali zilizotakiwa kupisha mradi

Maeneo yaliyolipwa fidia hadi kufikia mwezi Novemba alisema, ni Kata ya Kijichi,Kata Mbagala Kuu, Kata ya Mtoni, Kata ya Keko,Kata ya Kilakala, Kata ya Yombo Vituka, Kata ya Makangarawe,itakakojengwa Barabara ya Mchichani ,Barabara ya Chang'ombe, Barabara ya Temeke - Mbagala, Barabara ya Nzasa – Kilungule na Barabara ya Mwanamtoti. **Endelea uk.15**

Na waandishi wa habari



Joyce Msomba
Mhariri Mkuu /Msanifu kurasa wa jarida na Mhariri wa TMC TV
Afisa Uhusiano na Mkuu wa Kitengo cha Tehama



Nicodemas Masanja
Mwandishi na Mpiga picha
Mazoezini



Edda Mmari
Mhariri msaidizi wa jarida na TMC TV
Afisa Habari



Prisca Kikoti
Mwandishi na Mtangazaji
TMC TV
Mazoezini



Davina Majinge,
Afisa Tehama na Mshauri wa Masuala ya Mifumo



Beatrice Jonathan
Mwandishi na Mtangazaji
TMC TV
Mazoezini



Methew Jonas
Mchanganyaji wa habari
TMC TV
DSJ-DSM

Limetolewa na:
Ofisi ya Mkurugenzi,
S.I.P.46343
15533
DAR-ES-SALAAM
Simu: +255 22 292 8132
Faksi: + 255 22 292
Barua pepe : temeke@temekemc.go.tz
Tovuti : www.temekekemc.go.tz

YALIYOMO2. **Uongozi**3. **Waandishi wa jarida**4. **Yaliyomo**5. **Lyaniva : Mapato na matumizi kwa Manispaa**6. **Jukwaa la wanawake lazinduliwa**7. **Habari katika Picha**8. **Habari katika Picha**9. **Habari katika Picha**10. **Habari katika Picha**11. **Vijana waaswa kujitokeza kuchukua mikopo**12. **Tehama inavyoboresha ukusanyaji wa mapato**13. **Temeke Mpya ndani ya Dar-es-Salaam****TAHARIRI****TAKWIMU KWA MAENDELEO**

Kila mmoja wetu anaewela umuhimu wa kuhifadhi takwimu kikazi ama kijamii.

Ninaposema hivyo, leo hii kusingekuwa na historia kama waliotutangulia wasingejali kukusanya takwimu, kuzihakiki juu ya ubora wake na kuzihifadhi kwa njia mbalimbali walizotumia, leo hii zinatumika katika kazi zetu za kila siku.

Wito wangu kwenu; watumishi wenzangu, na wadau wa maendeleo, kila sekti iangalie upya ni nini kingefaa kuhifadhiwa katika kipindi hiki kwa manufaa ya baadaye pale zitakapohitajika, server ipo kwa Ngazi ya Halmashauri na Kitaifa ambazo zinauweweza wa kuhifadhi takwimu hizo (data base) inayosimamiwa na Kitengo cha Tehama, kwa manufaa ya vizazi vijavyo, na wafanyakazi wa baadaye.

Narudi kwenu, kuwaasa wakuu wa Idara na Vitengo kwa mara nyingine tena, muanda takwimu/taarifa/data zikiwemo idadi ya watumishi, na uongozi, idadi za vifaa, miundombinu iliyopo, matukio muhimu ya hali ya hewa, katika maeneo yenu ya kazi, aina za mazao yanayolimwa, Idadi na aina ya mifugo, Idadi ya wakazi na mengineyo kama hayo ili zihifadhiwe, kama-kumbukumbu ya kizazi hiki.

Mfumo wa kuhifadhi takwimu-database/upo, swala ni ninyi kusimamia uandaaji wa takwimu na kuwakabidhi wataalam wa kitengo cha Tehama.

TEHAMA NI KITENGO MTAMBUKA- TEMBELEA ULEKEZWA NI AINA GANI YA TAKWIMU/DATA ULETE ZIHIFADHIWE ,

"ANZA SASA"

JAFO: TEMEKE MPYA NDANI YA JIJI LA DAR-ES-SALAAM

Joyce Msumba

Nani asiyejua Temeke, Temeke iliyosikika kama ni ya wacheza ngoma ya tukumile, TUKUMILE ni ngoma zilizokuwa zikichezwa maeneo ya Tandika, chini ya mashamba ya mikorosho, ngoma hii ilikuwa maarufu sana Temeke, vilipo viwanja vya michezo hivi sasa Uwanja wa taifa na ule wa Uhuru, ilikuwa eneo la kuwinda wanyama wadogo wadogo kwa kitoweo, Temeke ile ya squatter na miundo mbinu mibovu; hivi sasa imebadirika sana. Hayo yalisimuliwa na Mzee Abdallah Maloka, Mkazi wa Temeke na mtumishi wa manispaa ya Temeke hadi hivi sasa.



**Utakumbukwa daima ,
Marehemu Mkurugenzi
wa kwanza wa
Manispaa ya Temeke,
Marehemu Idd Nyun-
do , aliyeibadirisha
Temeke na kuelekea
katika maendeleo ya-
nayoonekana hivi sasa.
" Kalale pema peponi "
Daima utakubwa na
wana Temeke**

Picture caption

Mtu aliyeondoka miaka hiyo akirudi ana-weza kupotea, Temeke ni nyingine siyo ile aliyoiacha, hayo yalisemwa na Waziri Ofisi ya



Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Selemiani Jafo, akiakabidhiwa ufunguo wa Jengo—Ofisi ya DMDP Manispaa ya Temeke

Akifafanua zaidi Waziri alisema; 'ilikuwa ikiniwi vigumu kuangalia chini wakati nikiwa angani ndani ya ndege ikielekea kutua, vijumba vidogo vya makuti, squatter, na barabara mbovu, hiyo ndiyo Temeke ya zamani, lakini hivi sasa, Temeke ina majengo ya maghorofa, ina viwanja vya michezo vikubwa, mtu yeyote awapo juu ndani ya ndege huvutiwa kuvian-galia kwa uzuri wake, ni mategemeo yangu kuwa wale walioondoka Temeke wakirudi baada ya mradi huu kukamilika wanaweza kupotea alisema.

Nianzie wapi kusema, Temeke ina historia kubwa ambayo haitampendeza Mungu endapo itasahaulika hivi hivi bila kusimuliwa kwa wajukuu zetu ama kuandikwa.

Mimi ni mmoja wa wahenga niliyeshuhudia mabadiliko haya, nilihamia Temeke miaka ya tisini, Temeke ile siyo hii tuionayo sasa, yenye barabara za lami, Taa za barabarani, maghorofa na hata maeneo tuliyokuwa tunaokota embe za mawazo na do-do hivi sasa yameota majumba makubwa.

Temeke ya Idd Nyundo, (Mungu amrehemu huko aliko), ndiye aliyeifungulia mlango wa maendeleo. Daima atakumbukwa.

Alianza kwa kujenga ofisi kubwa yenye sifa, jengo la ghorofa tatu, mtandao wa barabara za lami mfano mzuri, barabara ya Kichangani ambayo ilikuwa haipitiki kirahisi kutokana na kuwa na mchanga hata kuanzisha ajira kwa vijana waliokuwa wakikaa bure kutwa kunasua magari yaliyokwama pale hivi sasa imikuwa historia.

Vyumba vya madarasa vilivyojengwa, ununuvi wa madawati, Sekondari za Kata na vituo vya Afya, huo uliokuwa ni mwanzo tu wa mabadiriko ya Temeke mpya.

Kuja kwa Mradi wa uendelezaji miundombinu Jijini, (The Dar-es-Salaam Metropolitan Development Project-DMDP) utau-badirisha kabisa muonekano wa Temeke, na kuwa Temeke mpya ndani ya Dar-es-Salaam mpya.

Ni jambo la kumshukuru Rais Mstaafu Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kipindi chake cha uongozi, kwa kuipa upendeleo wa ziada Manispaa ya Temeke kuwa na miradi isiyopungua 13 yenye kufadhiliwa na

na Benki ya Dunia. Kati ya dola za Kiamerika Bilioni 600, — **Endelea UK 14**

TEHAMA INAVYOBORESHA UKUSANYAJI WA MAPATO

Davina Majige - TEHAMA

TEHAMA - Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Jukumu kubwa la kitengo ni kumshauri Mkurugenzi kuhusu masuala yote yahusuyo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuongeza tija kwa Manispaa.

Kitengo kinahusika na kusimamia, kuboresha na kuratibu mifumo mbalimbali, miundo mbinu pamoja na matumizi sahihi ya vifaa vya TEHAMA.

Manispaa ya Temeke inatumia mifumo ya TEHAMA kuboresha ukusanyaji wa mapato. Mfumo wa LGRCIS (Local Government Revenue Collection Information System) unatumika kuskanya mapato ya Halmashauri. Mfumo huu umeboresha uhifadhi wa taarifa muhimu za walipa kodi wote ndani ya Manispaa ya Temeke


ikiwemo taarifa kuhusu viwango vyao vya

malipo, mahali walipo walipa kodi hao pamoja na vipindi husika wanapotakiwa kulipia kodi zao.

Taarifa hizi zimerahisisha utoaji wa hati za madai kwa kila chanzo cha mapato na kwa kipindi husika.

Hali kadhalika mfumo unahifadhi taarifa za walipa kodi wanaodaiwa hivyo kurahisisha ufuatilaji wa wadaiwa sugu.

Mfumo wa mapato umerahisisha na kuboresha



Server—mashine ya kuhifadhi takwimu za mapato na taarifa muhimu za manispaa, Bibi Davina mtaalamu wa TEHAMA akihakiki taarifa kupitia Kompyuta iliyomo ndani ya chumba cha server

Hivyo ni rahisi kupata taarifa sahihi za wateja wote walipolipa kwa wakati.

Pia mfumo umeongeza uwazi na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kupunguza urasimu kwa kuboresha utaratibu mzima wa ulipaji kodi.

Matumizi ya vifaa vya POS (Point of Sale) ya merahisisha ukusanyaji wa mapato kwani walipa kodi wanaweza kulipa kodi mbalimbali katika ngazi ya kata hivyo kupunguza usumbufu katika ulipaji kodi.



LYANIVA: MAPATO NA MATUMIZI BORA KWA MANISPAA

Joyce Msumba

Simamieni matumizi ya fedha katika Kata zenu, msingoje kusomewa taarifa za mapato na matumizi na watendaji wenu, kwanza yawapasa mjue thamani ya miradi inayotekelizwa katika maeneo yenu ili mpate jinsi ya kuwaeleza wananchi, kwani wao wana kiu ya kuyajua hayo.

Hayo yalisemwa na Mhe. Felix Lyaniva Mkuu wa Wilaya ya Temeke, akioongea na baraza Maalum la madiwani kuhusu ukusanyaji wa mapato ya Manispaa.

Akiendelea Mhe. Lyaniva alisema; Wananchi wengi wa Temeke ni maskini, na vipato vyao ni vya chini sana, hivyo wasimamieni, hakikisheni wanapata elimu ya ujasiliamali na watafutiwe mikopo na masoko ya bidhaa zao.

Vile vile Mkuu huyo wa Wilaya alihoji kwa kusema; 'kwa nini mnataka kubinafsisha uendeshaji wa masoko, msikurupuke tu katika suala la ubinafshaji,



Mhe. Felix Lyaniva -Mkuu wa Wilaya

mnaweza kujikuta mnamfanya mtu biashara bure'.

Akitoa maelezo kuhusu hoja hii Mhe. Juma Rajab Mkenga, Naibu Meya alisema. Hilo lilizingatiwa, Kamati ya Fedha na Uongozi ilifanya ziara ya mafunzo na kupata uzoefu kutoka kwa wengine Manispaa ya llala na Mkoani Tanga juu wa ukusanyaji wa mapato, na hasa mapato yatokanayo na ushuru wa masoko kuhusiana na zoezi la ubinafshajji na jinsi wanavyonufaika.

Vile vile Mameneja wa mapato wamefanya utafiti wa kina katika ukusanyaji wa ushuru wa masoko kwa muda mrefu na wakaishauri Kamati ya Fedha kwamba hilo linawezekana. Kwa taarifa hiyo tangazo lilitolewa kupitia vyombo vya habari na kupatikana kwa mkandarasi atakayehusika na ukusanyaji wa ushuru huo kwa niaba ya Manispaa.

Kupitia Mifumo ya mapato pamoja na mashine za risiti za POS zitatumika na hivyo zoezi hilo ni salama Mhe Juma Mkenga alisema hayo.



Mhe.Kenny Makinda, Diwani wa Kata ya Makangarawe

Mhe. Juma Rajab Mkenga Naibu Meya alimpongeza Mhe. Kenny Makinda na kuwaomba waheshimiwa wengine kuiga mfano wake. Kwani yeze ameweza kuhamasisha wananchi wa Kata yake ya Makangarawe katika uchangiaji wa uzoaji taka ngumu kwa kukodisha magari na kuzisafirisha hadi dampo la Pugu Kinyamwezi.

Kwa zoezi hili limeipunguzia manispaa gharama ambazo ziliikuwa zikiletwa kwa kuondosha taka kutoka madampo ya muda kwa magari ya manispaa na yale yanayokodiwa na Serikali na kuzipeleka Pugu Kinyamwezi. Madampo haya ya muda yaliyokuwepo Temeke mwisho na Mwembe yanga yote yamefungwa hivi sasa.



Bwana Tumaini Mrango,
Mwekahazina wa Manispaa

JUKWAA LA WANAWAKE WAJASILIAMALI TEMEKE LAUNDWA

Edda Mmari

Bw.Hashimu Komba, ambaye ni Katibu Tawala Wilaya ya Temeke ameunda jukwaa la wanawake wajasiliamali walijitokeza kutoka kata zote kwa wingi katika ukumbi wa Iddi Nyundo uliopo hapa makao makuu ya Manispaa.

Kauli mbiu ya kikao hicho ni "Mwanamke tumia fursa kuimalisha uchumi wa viwanda" ambapo Katibu tawala huyo ameungana na juhudzi za Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu ikiwa ni mwendelezo wa uzinduzi wa majukwaa ya wanawake katika kuinua uchumi wa mwanamke ili kuleta Maendeleo kitaifa.

Kauli mbiu hiyo ilisemwa na Makamu wa Rais katika siku ya uzinduzi wa Jukwaa la uwezeshaji wa wanawake kiuchumi liliofanyika kimkoa .

katika viwanja vya Posta, eneo la kijitonyama. Uzinduzi huo ni wa 23 ndani ya Baraza lilioandaliwa kwa uwezeshaji wa ufadhili wa benki ya CRDB.

Akiongea na wanawake hao, Bw. Komba aliwamwagia sifa kwa juhudzi za kujikwamua kiuchumi katika jamii, aliwapongeza kwa namna wanavyo-jituma na kuwa waaminifu na uwezo wa kusimamia vipato vyao vidogo wanavyopata kwa kujileta maendeleo makubwa.

Aliahidi kuwa jukwaa hilo punde litakopoundwa litakuwa na tija kubwa katika kujitangazia biashara na ubunifu wa kazi zao wanazofanya katika ngazi za kimataifa, kitaifa, kimkoa, kiwilaya mpaka kata. Pia watapata fursa mbalimbali za kupiga hatua kama kushiriki maonesho ya kibishara ya sabasaba na nanenane.

Bw.Komba aliwasisitiza wanawake hao kuchagua viongozi wenye uwezo, mawazo, ubunifu na ujuzi wa kazi zao ili kusimamia jukwaa hilo katika kujiletea maendeleo

Hata hivyo amewapa moyo kuwa kwa kuelekea katika sera ya uchumi wa viwanda waendelea kutumia teknolojia ndogondogo wanazotumia nyumbani hivi sasa kuzalisha bidhaa mbalimbali ikiwa ni mfano yetu.



Bw.Hashim Komba akiongea na wanawake kuunda Jukwaa la Wanawake wajasiliamali



Baadhi ya Wanawake wajasiliamali waliohuduria kikao hicho



wa viwanda vidogovidogo, wakati wanajianda kupata viwanda vikubwa. Kwa kufanya hivyo watakuwa wanajingizia kipato pia kuinua uchumi wa viwanda katika nchi Katika kikao hicho, katibu Tawala alipongeza Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii inayoongozwa na John Bwana kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuwatambua wajasiliamali hao ambaa wamejitokeza kwa wingi na shauku kubwa kuunda jukwaa hilo.


Jukwaa hilo linatazamiwa kuzinduliwa hivi karibuni ikiwa lengo kuu ni kumwinua mwanamke kufikia katika uchumi wa kati, ambapo inasemekana mwanamke ni mlezi wa familia na jamii, ukimwezesha mwanamke imewezesha taifa.

"Jukwaa hilo punde litakopoundwa litakuwa na tija kubwa katika kujitangazia biashara na ubunifu wa kazi zao wanazofanya".

VIJANA JITOKEZENI KUCHUKUA MIKOPO

Nicodemas Masanja na Beatrice Jonathan

Vijana undeni vikundi vidogo vidogo na kuchukua mikopo kutoka Benki ya Wananchi ambayo itawasaidia kuijendeleza kiuchumi na hivyo kuondokana na umaskini na utegemezi kwenye jamii zenu.



Bw. Nassib Mmbagga Mkurugenzi

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Bw. Nassib Mmbagga alipokuwa akizindua mashine ya kutotolesha vifaranga katika kikundi cha vijana cha (Uhuru Jogging) Kata ya Buza wilayani Temeke

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Bw. Nassib Mmbagga awaomba wakazi wa maeneo hayo hasa vijana kufanya kazi kwa bidii na kuonesha mfano mzuri na kuwafanya watambulike na kujulikana kijamii na kiuchumi.

Aliongeza kuwa vijana ni nguvu kazi ya Taifa na hasa kuwataka vijana wa Temeke kuunda vikundi kama hiki cha Uhuru ambacho kina malengo zaidi ya kufanya mazoezi lakini kinachojishughulisha na shughuli za kiuchumi na hivyo kuchochea maendeleo yao kwa ujumla na kuwaomba waendelee kuwa imara zaidi.

Akikabidhi mashine hiyo Dokta Chesco Asheli ambaye



Dokta Chesco (aliyevaa suti) ambaye ndiye mbunifi wa mashine hiyo akiakabidhi kwa vijana mbele ya Mkurugenzi wa Manispaa (wa kwanza kushoto)

ndiye mbunifi na mtaalam wa mashine za kutotolesha vifaranga alisema; mashine hiyo ni ya kisasa na ina uwezo mkubwa wa kutotolesha vifaranga wa aina zote za ndege mpaka kufikia idadi ya 1656 ya vifaranga kwa siku, na aliongeza kuwa mashine hizo zipo za aina nyingi sana, kuna mashine zinazotumia umeme, mafuta ya taa ama betri.

Dokta Chesco aliwataka vijana wajiamini na wawe imara katika kufanya kazi kwa bidii na hivyo kuwafanya waondokane na umaskini wa jamii zao, kwani kazi huwafanya vijana wawe na vipato vyao.

Akimalizia Bw. Mmbagga aliwaasa vijana na wakina mama wachangamie fursa kwa kuchukua mikopo kwani mikopo ipo tayari benki ili wakopeshwe na



Baraza la Madiwani , likijadiri masuala ya upatikanaji wa mikopo kwa vijana, aliyesimama ni Mhe. W. Tarimo Diwani Kata ya Sandali

mikopo hiyo iweze kuwasaidia kufanya shughuli mballimi za kiuchumi na maendeleo kufanya maisha yao kuwa bora ili kujikwamua na umaskini.

Usikose kutufatilia kupitia mitandao yetu ya kijamii;

Website: www.temekemc.go.tz

Facebook: Temeke Manispaa

Twitter: temekemanispaa1

Blog : manispatemke.blogspot.com

Onlnetv: youtube TMC TV

UK.10 |

HABARI KATIKA PICHA

JULAI-DESEMBA 2017



Ofisi ya Mradi wa Dar-es-Salaam Meptropolitan Development Project, DMDP



Ujenzi wa barabara na daraja Mtaa wa
Mwanamtoti



Baraza la Madiwani la halmashauri ya Temeke, linalofanya kila
baada ya miezi mitatu likiongozwa na Mstahiki Meya Mhe. Abdal-
lah Chaurembo



Wanafunzi wa shule ya Msingi Maji Matitu, moja ya shule zilizozidi-
wa kwa kupokea wanafunzi wengi na uhaba wa vyumba vya
madarasa,pia madawati , sasa imebaki kuwa historia baada ya
kujengewa vyumba vya madarasa kumi na mijia na kupatiwa
madawati ya kutosha



Gari likipita katika moja ya mtaa Kata ya Kilakala,
ambako barabara hazipitiki kiurahisi, Kata hii
itanufaika na mradi DMDP

UK.7 |

HABARI KATIKA PICHA

JULAI- DESEMBA 2017



Mazingira mazuri yaliyotunzwa Manispaa ya Temeke



Mhe. Wilbrod Tarimo, aliyesimama akizungumzia masuala ya
ukusanyaji wa Mapato katika Baraza la madiwani



Barabara mpya ya Kivungo-Kata ya Tandika, imerahisisha
usafiri wa mabasi makubwa na madogo yafikayo kuchukua
abiria kituo cha Tandika Mwishi



Timu ya bajeti ikiandaa Mpango mkakati (Strategic Plan) kwa



Mhe. Isaya Mwita Meya wa Jiji la Dar-es-Salaam, wa kwanza
kushoto, akiongozana na Mhe Abdallah Chaurembo Meya wa Manispaa



Zahanati ya Charambe– kata ya Charambe

UK.8 |

HABARI KATIKA PICHA



Mhe. Selemani Jafo, (katikati) akizindua Jengo la Ofisi Mpya ya DMDP lililoko Manispaa ya Temeke



Ujenzi wa nguzo za daraja la Kijichi Toangoma



Makabidhiano ya Mkataba uliosainiwa kwa Miradi ya awamu ya pili wa DMDP



Mratibu wa Mradi wa DMDP Bwana Edward Simon mwenye kofia nyekundu akifanya kazi na fundi wa ujenzi kwenye daraja la Kijichi Toangoma



Uandikishaji wa vitambulisho vya Afya wa Wazee katika ofisi za Kata

JULAI-DESEMBA 2017

UK.9 |

HABARI KATIKA PICHA



Majengo ya shule ya Msingi Rufu kata ya Chamazi



Malipo yote sasa kufanyika kwa njia ya Kielektronik, kupokea mapato ya ndani. Hizo ni shughuli ndani ya tawi la Benki ya CRDB lililopo Jengo la kuu la Utawala Manispaa ya Temeke. Picha na Joyce Msomba



Michezo kwa Afya, watumishi wa manispaa ya Temeke wakifanya mazoezi katika kiwanja cha Sekondari ya Kibasila, kila siku ya ijumaa




Mhe. Seleman Jafo, Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, akabidhiwa ufunguo wa kuzindua jingo la Ofisi ya DMDP Manispaa ya Temeke



Mhe. Felix Lyaniva, aliyekaa katikati, akizungumza na kamati ya usimamizi wa uchangiaji damu salama katika Vituo vya Afya



Wenyeviti wa kamati za Kudumu; kutoka kulia ni Mwenyekiti kamati ya Mipango Miji na Mazingira, na Kushoto ni Mwenyekiti kamati ya Uchumi, Afya na Elimu.



Watumishi Ofisi ya TEHAMA_Uhusiano wakiwa kazini katika uingizaji wa taarifa kwenye tovuti

JULAI -DESEMBA 2017